Barry, A. L. - WHAT ABOUT? DEATH AND DYING
- Swahili

Kuhusu Jambo Gani...

# Mauti Na Kufa

**Daktari A. L. Barry**
**Rais**
**Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri**

THE LUTHERAN CHURCH – MISSOURI SYNOD

Salamu kwa jina la Yesu Kristo Bwana wetu. Kama Wakriso, tuna maono ya pekee kuhusu mauti, maono yaliyo tofauti kabisa na ulimwengu unaotunzunguka. Kusudi la kabrasha (pamphlet) hili ni kukusaidia, au kumsaidia mtu fulani unayemjua, akabiliane na ajue mauti ni nini, na namna Wakristo hukabiliana na mauti na wanavyoshughulikia huzuni.

**Mauti ni Nini?**

Biblia hufundisha kwamba, mauti si maangamizi ambayo kwa hayo kuwepo kwetu kunakoma. Maandiko Matakatifu hufundisha kwamba, mauti ni utengano wa roho yetu ya milele na miili yetu inayokufa. Miili yetu hupumzika kaburini, ikisubiri siku ya mwisho wakati roho na mwili vitaunganishwa. Wakati wa mauti, roho zetu, na roho za wale ambao wanakufa katika imani, huwa mbele ya Kristo mara moja, na zitafurahia uwepo Wake, amani na furaha mpaka siku kuu ya kufufuka kwa miili yote.

**Je, Mauti ni Jambo la Kawaida?**

Ni rahisi kuyafikiria mauti kama jambo la "kawaida." Hata baadhi ya watu wamesikika wakisema, "Mauti ni rafiki." Hakuna ukweli ushindao huo. Mauti ni ukweli wa kutisha. Ni adui anayemkabili kila mmoja wetu mwishoni mwa maisha yake. Mauti ni laana mbaya ambayo iliushambulia uumbaji kwa njia ya dhambi ya Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni. Kwa njia ya dhambi hiyo, mauti yaliingia ulimwenguni na hivyo yakawapata wanadamu wote kwa sababu watu wote hutenda dhambi.

Mungu hakuwaumba wanadamu wafe, bali [aliwaumba] wawe hai wawe hai milele na wamfurahie Yeye milele. Mauti hayakuwa sehemu ya kuumbwa kwetu kwa asili, bali tendo lililokuja kama matokeo ya dhambi ya uasi wa wazazi wetu wa kwanza, dhambi ya uasi ambayo ilirithishwa kwa kila mwanadamu tangu wakati huo.

**Kwa Nini Wakristo Hufa?**

Maandiko Matakatifu huonyesha wazi kwamba, Wakristo pia lazima wapitie mautini ili waingie uzimani. Tunajifunza kwamba, hakika miili yetu imekufa sasa kwa sababu ya dhambi "Mwili wenu umekufa kwa sababu ya dhambi" (Warumi 8:10). Na kwa hivyo Wakristo pia lazima wafe.

Uchungu wa mauti na ufahamu wa hukumu ya Mungu ni adhabu za kutisha sana kwa wale wasiomwamini Kristo kama Mwokozi wao. Mwishoni mwa maisha yao, hukabiliana tu na tarajio la wakati ujao usiojulikana, au maono ya kutisha ya laana ya milele. Hata hivyo, kwa ufahamu mtimilifu, mauti ya Mkristo si mauti kama yalivyo kwa wasiokuwa Wakristo. Kwa Mkristo, uzima wa milele na furaha huyafuata mauti. Maana Bwana wetu Yesu Kristo ndiye anayepita nao kwenye "bonde la uvuli wa mauti" (Zaburi 23).

**Je, Jibu la Mkristo ni Lipi kuhusu Mauti na Kufa?**

"Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya." Maneno haya yajulikanayo kutoka Zaburi 23 huonyesha mwelekeo kwa Mkristo binafsi au familia inayokabiliwa na ukweli wa mauti. Hapa, Mungu humtambua adui yetu mkuu nyakati kama hizo woga. Kwa kuwa hakuna hata mmoja miongoni mwetu aliye hai aliyewahi kuonja mauti, jibu la tarajio letu kuhusu mauti (yawe ni yetu wenyewe au ya mtu tumpendaye) ni la woga. Woga ni jambo la kawaida.

Sasa, ikiwa woga ni adui, ni nani aliye upande wetu? Mwandishi wa Zaburi huendelea: "Kwa maana Wewe upo pamoja nami, Gongo [L]ako na Fimbo [Y]ako vyanifariji." Yesu, Mchungaji wetu Mwema, Yeye ambaye aliutoa uhai Wake

kwa ajili ya kondoo, ndiye rafiki yetu aliye katika njia ya mwisho yenye giza, ipitayo kati ya bonde la uvuli wa mauti. Safari hii si ya hiari. Siku moja kila mmoja wetu, awe mzee au kijana, ataipitia njia hiyo. Haya yataendelea mpaka siku ile Yesu atakuja tena wakati, parapanda ya mwisho ikilia, watakatifu watabadilishwa kufumba na kufumbua (1 Kor. 15: 51-52).

Lakini hapa kuna sehemu muhimu: Nitapita kati ya uvuli. Yeye aliye pamoja nasi katika safari hiyo, atuongozaye, ana majeraha ya mauti katika mwili Wake wenye uhai. Alikuwa amekufa, bali sasa yu hai milele. Wote waaminio na kubatizwa wataokoka; wana sehemu katika ushindi Wake dhidi ya mauti. Kwa hiyo, Wakristo wanaweza kuyaona mauti siyo tu kama ukweli wa kusikitisha unaotakiwa kuvumiliwa, bali kama adui aliyeshindwa. Kufufuka kwa mwili na uzima wa milele ndizo hakika imara na thabiti zilizoahidiwa wote wanaobaki kuwa watakatifu mpaka mautini.

**Nini Hutendeka baada ya Kufa kwetu?**

Kwa wasioamini, kuna "mauti ya pili" (Ufu. 20:14) ambapo roho zao zitakuwa mbele ya Shetani na mara moja wataanza kuteseka kwa kusumbuliwa na adhabu ya milele katika jehanum, ambamo kutoka humo, haitawezekana kutoroka. Siku ya hukumu, miili yao itaungana na roho zao katika jehanum.

Wale wanaotegemea ukombozi alioushinda Kristo Bwana wetu hupitia mautini kuingia uzimani. Hii ndio sababu Biblia hutumia taswira nyingi sana za kufariji ili kuelezea mauti ya Mwana wa Mungu. Hivi ni baadhi ya virai (phrases) anavyovitumia Roho Mtakatifu ili kuyaelezea mauti ya Mkristo: kukusanyika mbele Zake; kwenda kwa amani; kwenda na kukaa pamoja na Kristo; kujiepusha na uovu utakaokuja; kulala; kupumzika; kupitia mautini na kuingia uzimani; kuokoa kutoka katika maovu yote; na mwisho, "kufaidi."

Kufaidi? Mauti yanawezaje kuwa kufaidi? Wakati mtoto wa Mungu aliyebatizwa anapitia mautini – mwanawe au bintiye Mungu ambaye amekombolewa kwa damu ya Mwana-kondoo wa Mungu – basi, kwake mauti ni kufaidi. Kwa njia ya mauti, watoto wa Mungu huingia katika furaha na amani ya milele kuwa na Baba yao aliye mbinguni.

Kwa hiyo, kila Mkristo anaweza kufurahia maisha ambayo Kristo amemshindia na kumpatia yeye kwa njia ya Neno na Sakaramenti. Tunapokufa, roho zetu hungojea kuharibiwa milele kwa vitu vyote siku ile Kristo atarudi. Tutapokea miili iliyotukuzwa ambayo haina machozi, huzuni, magonjwa na uzee miili ya kufufuliwa iliyo mipya na iliyotukuzwa kabisa.

Katika miili hii mipya iliyotukuzwa, tutaishi mbinguni milele, tukifurahia mbele za Mungu pamoja na watakatifu Wake wote, milele na milele. Furaha kuu sana ya ukweli huu, ni zaidi kwetu hata kuanza kuifahamu, lakini ni kweli!

**Wakristo Wanakabilianaje na Mauti?**

Wakristo hukabiliana na mauti namna wanavyokabiliana na maisha – macho yao yakimtazama Yesu sana. Tunashikilia ahadi za Neno Lake sana, ambazo, tunapokabiliana na mauti, huonekana kuwa za ajabu na zenye nguvu zaidi. Ahadi mojawapo nzuri sana aliyotupatia Bwana inapatikana katika Yohana 14:2-3 ambapo husema, "Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi [M]imi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe [K]wangu; ili nilipo [M]imi, nanyi mwepo."

Tunatambua kwamba, haidhuru maisha yetu yatakavyofikia kikomo, kuna jambo moja ambalo tuna hakika kwalo. Tutapitia mautini na kuingia uzimani, tutatoka kutoka maisha haya na kuingia paradiso pamoja na Bwana. Na huko tutaungana na wapendwa wetu wote na wengine ambao walikwisha kututangulia wakimtegemea Kristo Mwokozi wao.

**Mkristo Anashughulikiaje Huzuni?**

Wakristo hawapaswi kusita kulia. Bwana wetu alilia kwenye kaburi la rafikiye Lazaro. Nasi pia tunajipata tukilia kwa huzuni ya kufiwa. Lakini hatuhuzuniki kwa njia ile ile ya wale wasiokuwa na matumaini. Ikiwa tunaamini kwamba, alikufa na kufufuka tena, vivyo hivyo, kwa njia ya Yesu, Mungu atawaleta pamoja na Yeye wale waliolala (1 Tes. 4:14). Tunasubiri muungano ule mkuu pamoja na wapendwa wetu waliokufa kwa imani. Bado tunawakosa. Utengano huu unaweza kutulemea nyakati zingine. Huzuni hii ni sehemu ya mzigo wa kuomboleza; unapaswa kufahamika, sio kupingwa.

Kwa watu wengi, kulia ni safari. Ni safari kutoka kwa uchungu wa kwanza wa kufiwa, mpaka kwenye kupona na kupatanishwa na kufiwa kwetu. Uchungu hupungua pole pole, lakini hasara ya kufiwa hubaki. Huzuni ina viwango vingi na inaweza kuonekana isiyotabirika katika kupungua na kuongezeka kwake; ilihali katika Kristo tunapata nguvu tunapokuwa safarini. Maana hatuko peke yetu katika safari hii.

Wakristo hutambua kwamba, familia na marafiki ni vipawa vya Mungu vya kuwasaidia wavumilie uchungu wa kufiwa, ambao huonekana kutovumilika wakati mwingine. Ushirika wa aina hiyo ni muhimu kwa kuishughulikia huzuni kwa njia inayofaa. Lazima wale wanaoomboleza wautafute kwa kujitambulisha. Wengi wanaoomboleza hupata msaada wanapoambia familia na marafiki wanaowategemea historia ya wafu wanaowapenda. Kusimulia historia hiyo tena na tena huleta faraja na ufahamu katika furaha na huzuni ya kufiwa. Marafiki na watu wa familia watataka kusikia na kusikitikia masimulizi ya aina hiyo tena na tena. Ni nafasi ya pekee kupatiwa hazina ya aina hiyo. "Mchukuliane mizigo na kuitimiza hiyo sheria ya Kristo" (Gal. 6:2).

Zaidi ya yote, Wakristo waombolezaji watakimbilia ushirika wa ibada ya kanisa na wingi wa faraja ya Neno takatifu na Sakramenti ya Mungu kwa kuwaponya katika safari ya huzuni. Maana Yesu Kristo hukaa katika kanisa Lake kwa njia ya vyombo vya neema vitakatifu Vyake. Kwa njia hivyo, Yeye hutoa utajiri wa msamaha Wake, uzima na wokovu sasa, na milele na milele. Siku moja nasi pia tutasimama na umati huo mkubwa wa mbinguni ambao husikia maneno haya ya kubarikiwa:

"Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, [N]aye atafanya maskani [Y]ake pamoja nao, nao watakuwa watu [W]ake. Naye Mungu [M]wenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita" (Ufu. 21:3-4).

Daktari A. L. Barry
Rais
Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri